An official website of the European Union How do you know?

Hatua zilizochukuliwa na Umoja wa Ulaya ili kuboresha usalama wa chakula ulimwenguni

Umoja wa Ulaya unachukua hatua ili kuhakikisha kwamba usalama wa chakula ulimwenguni unarejeshwa kupitia ushirikiano wa kimataifa. Pia tunaandaa msaada wa kibinadamu na usaidizi kwa wakulima walioathirika zaidi.

Msaada wa €210 milioni wa chakula kwa ajili ya walio wanyoge zaidi duniani

Kufuatia kipya cha msaada wa kibinadamu cha €210 milioni kitatolewa katika nchi 15, kiwa ni hatua za kamati kuongeza msaada wa kusaidia wale walioathirika kwa kiasi kikubwa zaidi na athari za uhaba wa chakula zinazozidi kuongezeka ulimwenguni kote. Kwa ujumla msaada kutoka EU (Umoja wa Ulaya) wa uhakika wa kupata chakula duniani kote sasa unafika €8 bilioni, kati ya 2020 hadi 2024.

"Uvamizi wa Urusi dhidi ya Ukraine umeleta athari duniani kote. Inahusiana na maisha na riziki za mamilioni ya watu duniani kote ambao wana hofu kuwa hataweza kumudu gharama za kupasha joto makazi yao au kuwapatia chakula watoto wao."

Ursula von der Leyen, Raisi wa Tume ya Ulaya

Uchokozi wa Urusi unasababisha mzozo wa chakula ulimwenguni

Uvamizi wa Urusi dhidi ya Ukraine umekuwa na athari ya haraka kwa usalama wa chakula kwa mamilioni ya watu kote ulimwenguni. Gharama kwenye mnyororo wote wa uzalishaji wa chakula zimeongezeka. Ongezeko la gharama za nishati na mbolea limedhoofisha masoko ya kilimo, na mtiririko wa kibiashara kuelekea na kutoka Ukraine na Urusi umevurugwa.

Nchi ya Ukraine peke yake huzalisha zaidi ya nusu ya ngano inayosambazwa na Mpango wa Chakula Duniani. Ufyatuaji wa risasi na makombora unaharyna wakulima wa Ukraine washindwe kupanda mbegu.

Urusi kwa makusudi inalenga na kuharibu mashine za kilimo, hifadhi ya chakula, na miundombinu ya usindikaji na usafirishaji wa chakula nchini Ukraine.

Urusi inazuia usafirishaji wa chakula chake nje ya nchi na pia inazuia mamia ya meli zilizobeba ngano katika Bahari Nyeusi.

Vikwazo vya Umoja wa Ulaya vilivyowekwa dhidi ya Urusi na Belarus havijaleenga sekta ya kilimo. Ununuzi, uagizaji na usafirishaji wa bidhaa za kilimo na chakula haupo kwenye marufuku iliyowekwa dhidi ya meli zenye kupeperusha bendera ya Urusi.

Jibu la Umoja wa Ulaya

Umoja wa Ulaya kama mshirika wa muda mrefu na wa kutegemewa kwa nchi nyingi duniani kote, inafanya kazi ili kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula duniani na kujenga mifumo thabiti ya chakula.

Upatikanaji wa chakula kwa sasa hauko hatarini katika Umoja wa Ulaya, kwa kuwa bara hilo linajitosheleza kwa bidhaa nyingi za kilimo. Hata hivyo, sekta yetu ya kilimo huagiza kwa ujumla bidhaa maalum, kwa mfano protini za mafiaho. Udhaifu huu, pamoja na gharama kubwa za pembejeo, kama vile mbolea na nishati ya visukuku, husababishia changamoto za uzalishaji kwa wakulima na hatari ya kupanda kwa bei ya vyakula.

Tume ya Ulaya inapendekeza hatua mbalimbali za muda mfupi na wa kati ili kuimarisha usalama wa chakula duniani na kusaidia wakulima na walaji katika Umoja wa Ulaya katika kipindi ambacho kuna hali ya kupanda kwa bei ya vyakula na gharama za pembejeo.

Tunafanya yafuatayo:

- tunasaidia kusafirisha nafaka kutoka Ukraine
- tunasaidia watu walio katika mazingira magumu
- tunaongeza uzalishaji wetu wa chakula
- tunaondoa vikwazo vya biashara ya chakula na kukuza ushirikiano na pande mbalimbali

Tunaimarisha usalama wa chakula duniani

€8 bilioni

zimewekezwa na EU kwa ajili ya uhakika wa kupata chakula duniani (2020-2024)

Zaidi ya nchi 70

zitasaidiwa katika kuongeza ustahimilivu wa mifumo yake ya chakula

Athari za kimataifa kutokana na kupungua kwa uzalishaji wa mazao

Kupungua kwa uzalishaji na mauzo ya nje ya mazao kutoka Urusi na Ukraine kunaleta hatari kubwa ya upatikanaji wa chakula na uwezo wa kumudu gharama katika maeneo yaliyo jirani na Umoja wa Ulaya katika Afrika ya Kaskazini na Mashariki ya Kati, lakini pia katika Asia na Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hili linahusisha hasa ngano, ambayo ni chakula kikuu cha maingi.

Tume imejitolea kuchukua hatua zote muhimu ili kuhakikisha kwamba Umoja wa Ulaya, kama muuzaji wa jumla wa chakula nje na mzalishaji mkuu wa mazao ya kilimo cha biashara, inachangia usalama wa chakula duniani. Umoja wa Ulaya unaongoza kwa kutoa msaada wa kibinadamu na maendeleo kwenye mifumo ya chakula na chakula.

Kuna uwezekano mkubwa kwamba mahitahi na gharama za kinadamu vyote vitaongezeka na kuongeza shinikizo kwa msaada wa kibinadamu. Tangu 2015, EU imetumia sio chini ya €350 milioni, kwa mwaka, kwa ajili ya msaada wa chakula wa kibinadamu. Kati ya 2020 na 2024, EU inawekeza €8 bilioni kwa ajili ya uhakika wa kupata chakula duniani. Katika kipindi cha 2021 hadi 2027, EU itasaidia mifumo ya chakula katika takriban nchi mbia 70.

- Mnamo tarehe 6 Aprili, Umoja wa Ulaya na Nchi Wanachama zilahidi zaidi ya €1 bilioni kushughulikia usalama wa chakula katika ukanda wa Sahel.
- Mnamo tarehe 26 Aprili, Umoja wa Ulaya na Nchi Wanachama zilahidi €633 milioni kwa ajili ya msaada wa haraka na kuimarisha mifumo ya chakula na ustahimilivu katika Pembe ya Afrika.
- Mnamo tarehe 24 Septemba, EU ilitoa €600 milioni kwa nchi zilizo za unyonge zaidi, za Afrika na za Visiwa vya Karibi na Pasifiki, zilizokumbwa na janga la uhaba wa chakula.
- Mnamo tarehe 14 Novemba, Kamati iliitangaza kifunahi kipya cha msaada wa kibinadamu cha €210 milioni kwa ajili ya nchi 15, zilizoathirika kwa kiasi kikubwa zaidi na athari zinazoendelea kuogezeka za uhaba teketezi wa chakula.

Kwa ukanda jirani wa Kusini, Umoja wa Ulaya umepitisha fungu la msaada wa €225 milioni ili kupunguza athari za mgogoro ya chakula inayoweza kutokana na ulegemezi mkubwa wa uagizaji wa chakula ambao umevurugwa na vita.

Zaidi ya hayo, Umoja wa Ulaya kwa nguvu zote utaendelea kupigania kuepuka vikwazo vya kuuza nje na kupiga marufuku usafirishaji wa chakula, pamoja na kutengenezea soko la pamoja linalofanya kazi kwa ufanisi.

Mgogoro huu mkubwa unathibitisha kwamba tunahitaji kuharakisha mchakato wa mabadiliko ya mifumo wa chakula duniani kote kwa kuelekea kwenye mfumo endelevu na thabiti ili kujiandaa vyema kwa majanga yajayo. Kama ufuatiliaji wa Mkutano wa Umoja wa Matafa wa Mifumo ya Chakula wa mwaka 2021, Tume inashiriki katika miungano minane ya kimataifa ambayo yote inalenga kuleta mabadiliko ya mfumo wa chakula, ustahimilivu na kuongeza uzalishaji endelevu wenye tija.

Msaada kwa Ukraine

Umoja wa Ulaya unafanya kazi kwa bidii ili kuweza kuondoa nafaka iliyozuiwa nchini Ukraine iweze kufika katika masoko ya kimataifa, ili kuweza kuwapatia watu wa Ukraine kipato wanachohitaji sana na pia kuweza kuupatia Mpango wa Chakula Duniani mahitaji unayohitaji sana.

Umoja wa Ulaya unafungua njia za mshikamano na kufadhili njia tofauti za usafirishaji ili nafaka ya Ukraine iweze kufika nchi zilizo hatarini zaidi duniani.

Njia za Kimshikamano za EU

Shoroba kuu za Ukraine za mahuruji ya kilimo

Tani milioni 15

Mahuruji ya bidhaa za kilimo kutoka Ukraine kwa msaada wa njia za kimshikamano za EU

€1 bilioni

Imewekezwa na Kamati ya EU na wabia wake ili kuendeleza na kuipa msukumo uwezo wa shoroba

Umoja wa Ulaya pia unaongeza uzalishaji wake ili kupunguza shinikizo kwenye masoko ya chakula duniani, na unafanya kazi na Mpango wa Chakula Duniani ili hifadhi ilyopo na bidhaa za ziada ziweze kufikia nchi zilizo hatarini kwa bei nafuu.

Tume ya Ulaya pia inalunga mkono Ukraine katika kuandaa na kutekeleza mkakati wa muda mfupi na wa kati wa usalama wa chakula ili kuhakikisha kwamba michango inafika mashambani pale inapowezekana, na kwamba vyombo vya usafiri na uhifadhi vinatunzwa ili kuwezesha nchi hiyo kufisha raia wake na hatimaye kurejeshia uchibiti wa masoko lake ya nje.

Msaada kwa wakulima wa Umoja wa Ulaya

€500 milioni zitasambazwa katika mgao wa kitafa ili kusaidia moja kwa moja wakulima walioathirika zaidi na gharama kubwa za pembejeo na kufungwa kwa masoko ya nje. Nchi za Umoja wa Ulaya zinaweza kukamilisha usaidizi huu hadi 200% kwa fedha za kitafa.

Ili kushughulikia matatizo ya muzunguko wa fedha yanayowakabili wakulima kwa sasa, nchi za Umoja wa Ulaya zitaruhusiwa kulipa viwango vilivyoongezwa vya malipo ya moja kwa moja ya CAP mapema.

Tume imeke isha:

- imekeisha kutoa kibali maalumu na kisicho cha moja kwa moja kwa kushusha hadhi ya ardhi iliyotengwa ndani ya Umoja wa Ulaya ili kuruhusu uzalishaji wa mazao kwenye ardhi hiyo, huku ikihakikisha malipo kamili kwa wakulima watakaotumia njia za kilimo rafiki
- imependekeza Mfumo mpya wa kukabiliana na Migogoro ya Muda Mfupi ambao pia utajumuisha wakulima, wazalishaji wa mbolea na sekta ya uvuvi

Tume pia itaanzisha hatua za jumla za usalama wa soko ili kusaidia soko la nyama ya ngururwe kwa kuzingatia hali ngumu inayokabiliti sekta hiyo.

Msaada kwa walaji wa Umoja wa Ulaya

Hatua za kuboresha usambazaji wa vyakula vikuu zitasaidia kupunguza shinikizo la bei.

Nchi Wanachama wa Umoja wa Ulaya pia zinaweza kutekeleza punguzo la viwango vya kodi ya ongezeko la thamani na kuhimiza waendesha uchumi kudhibiti bei za rejareja.

Zaidi ya hayo, Nchi Wanachama zinaweza kuchukua fedha kutoka kwenye mifuko ya Umoja wa Ulaya kama vile Mfuko wa Kuzisaidia Nchi za Umoja wa Ulaya Zilizoathirika Zaidi (FEAD) ambayo inasaidia hatua za nchi za Umoja wa Ulaya kutoa chakula na/au usaidizi wa kimsingi kwa wallioathirika zaidi.

Ustahimilivu na uendelevu wa mifumo yetu ya chakula

Kulmarisha ustahimilivu kwa kupunguza utegemezi wa kilimo cha Ulaya kwenye nishati, uagizaji wa kiasi kikubwa cha nishati na uagizaji wa malisho kwa kasa ni jambo la muhimu zaidi kufiko hapo awali. Ustahimilivu unahitaji kuwa na uyanzo mseto vya kuagiza kutoka kwenye masoko ya nje na milango ya kimasoko kupitia sera thabiti ya biashara ya pande nyingi na baina ya nchi mbalimbali.